

102/3  
KISWAHILI  
FASIHI  
KARATASI YA 3  
JULAI/AGOSTI 2011  
MUDA: 2 ½

# MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA YA SHULE ZA WILAYA YA NYAMIRA

*Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya. (K.C.S.E)*

**Kiswahili  
Fasihi**

## MAAGIZO

- Jibu maswali **manne** pekee
- Swali la kwanza ni **lazima**
- Maswali hayo mengine **matatu** kutoka sehemu **nne** zilizobaki yaani, tamthilia, riwaya, Ushairi na fasihi simulizi.
- Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja.

Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

**SEHEMU YA A: HADITHI FUPI**

**MAYAI WAZIRI WA MARADHI: K.W Wamitila.**

**1. LAZIMA**

“..... Ni.... Nisubiri kidogo mpenzi..... naja hivi punde... tuyamaliza uyasemayo.”

- a) Eleza muktadha wa dondo hili. (ala 4)
- b) Anayosema mnenewa yanaashiria matatizo yanayomkumba. Jadili kwa kutoa mifano kitabuni manne ya matatizo hayo ambayo pia ni matatizo yanayoikumba jamii. (ala.8)
- c) Ni vipi matatizo hayo yanavyoweza kusuluhishwa? (ala.8)

**SEHEMU YA B : RIWAYA**

**S.A Mohamed : UTENGANO**

**Jibu swali la 2 au la 3**

2. “ Shoga Futoni ni Futoni kweli, mambo yake ni mfutofuto, hakuna mtaji mkubwa hata hivyo kwa mimi na wewe.....”.
- a) Eleza muktadha wa dondo hili. (ala.4)
- b) Eleza jinsi njia alizotumia kujipatia riziki mnenewa zilivyomtia mashakani (ala. 10)
- c) Eleza jinsi mnenewa hakubadilisha maisha yake. (ala.6)

**au**

3. Huku ukitoa mifano onyesha jinsi mwandishi amefaulu katika matumizi ya mbinu zifuatazo za sanaa:
- (i) Rejea (ala.10)
- (ii) Sadfa (ala.10)

**SEHEMU YA V: USHAIRI**

4. **Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.**

**UTII**

Raia Mwema ni yule, aliyejaa utii,  
Si ubishi na kelele, akanywalo hasikii,  
Ni mwasi huyo jinale, achunguzwe kwa bidii,  
Raia asiyetii, ni fisadi wa nchiye

Uonapo uhalifu, usambe huuzuii,  
Ndio huo uvunjifu, kamawe huzingatii  
Mwananchi mwadilifu,hilo halikadirii  
Raia asiyetii, ni fisadi wa nchiye

Utii kama haupo,sheria haziagii

Imani huwa haipo, na mema hayatujii  
Usalama hufa papo, mara nchi ikadhii  
Raia asiyetii, ni fisadi wa nchiye

Nia za watu watano, ambazo hazififii  
Uchao ni tangamano, si chusa hawachukii  
Hushinda kumi na tano, ambao hawatulii  
Raia asiyetii, ni fisadi wa nchiye.

Kila raia nchini, ni ile au ni hii  
Anachisa wastani, ingawa haitumii  
Hazuiliwi hanani, kusema hatumbukii  
Raia asiyetii, ni fisadi wa nchiye.

**Maswali.**

- (a) Taja sifa mbili za raia Mtiifa. (ala. 2)  
(b) Ni mambo gani ambayo hutokea wananchi wanapokosa utii? (ala.2)  
(c) Eleza ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari (ala. 4)  
(d) Onyesha mbinu mbili zilizotumiwa ili kuonyesha uhuru wa mtunzi, kwa kutolea mifano. (ala.2)  
(e) Hili ni shairi la aina gani? Toa sababu. (ala.2)  
(f) Eleza muundo wa shairi. (ala. 4)  
(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi. (ala.4)  
(i) Mwasi  
(ii) haziagii  
(iii) Tangamano  
(v) hisa

**5. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.**

**Wana –haramu**

Hebu nikuulize mama Afrika  
Kwa nini.....  
Mimba changa ukajichukulia  
Ya haramu sana ilotepetea  
Ukaza wana walo jahilia  
Wasiojijua, wala yao njia ?

Kuzurura ukamalizikia  
Bila muruwa, heba kukupotea  
Ukawa ganda la kupita njia  
Usije maoni ya kuonelea?

Kwa nini.....  
Ukaza kizazi kilo kiwete  
Kilihasirika kwa wakati wote  
Kilichopagawa kwa kingi kite

Hata utu wake ukakipotewa?

Ah moyo waumia!  
Hupigwa na mshangao  
Niwafikiriapo  
Wale barobaro wanao.  
Wasaliti wanati walo na vyeo  
Walomdhidi magha mzazi wao  
Kwa muradi wao.

Lakini sijali  
Sijali kwani najua  
Siku moja itawadia  
Wanaharamu watajihalalia  
Kila cha haramu kukuondolea  
Na kukurakasa.....  
Mama wasikia?  
Hiyo siku ya siku itakapofika  
Kila la dhuluma litajikatika  
Na kila mahali utadhihirika  
Mwisho wa salata na uharamia.....  
Mama wasikia?

### **Maswali**

- (a) mwandishi analalamikia mambo yapi katika shairi hili? (ala.5)
- (b) Mwandishi ametumia mbinu gani katika kutumia maneno. “Mama Afriaka?” Neno hili limetumika kumaanisha nini? (ala. 4)
- (c) Andika ubeti wa nne katika lugha ya nathari. (ala.4)
- (d) Eleza maana ya maneno yafuatayo: (ala 5)
- (i) jahilia (ii) Muruwa  
(iii) Kilohasirika (iv) kite  
(v) Barobaro.
- (e) Mtunzi anamaanisha nini anaposema, ‘ukazaa kizazi kilo kiwete?’ (ala. 2)

### **SEHEMU YA C : THAMTHILIA**

#### ***KIFO KISIMANI: Kithaka wa Mberia***

6. Huku ukitoa mifano jadili mambo mbalimbali yanayodhinisha ubaya wa utawala wa Mtemi Bokono. (ala. 20)

**SEHEMU YA D: FASIHI SIMULIZI.**

7. (a) Kwa kutoa mifano taja mambo yoyote manne yanayozua lakabu (ala.4)  
(b) Jadili kwa kutoa mifano, umuhimu wa lakabu (ala.8)  
(c) Eliza sifa zozote nne za lakabu (ala.8)

For More Free KCPE Revision Past Papers and answers  
Visit <http://www.freekcpepastpapers.com>